



NYONGEZA YA 1 YA KITABU CHA TAARIFA KWA WAOMBAJI WA ULINZI WA KIMATAIFA (IPO 1)

Sehemu ya 8 - Haki zako na wajibu katika Mchakato wa Ulinzi wa Kimataifa

Upatikanaji wa Soko la Ajira

Upatikanaji wa soko la ajira kwa waombaji wa ulinzi wa kimataifa umewezeshwa na Ireland kuchagua kuingia ndani ya EU (mara ya nyingine) Maagizo ya Masharti ya Mapokezi (2013/33EU).

Kanuni Zilizopitishwa na Ireland kama matokeo ya Maagizo hayo zinaruhusu ufikiaji mzuri wa masoko ya ajira pale ambapo hakuna pendekezo la kwanza la maombi ya ulinzi wa kimataifa lilofanyika ndani ya miezi 6.

Mwombaji wa ulinzi wa kimataifa anaweza kupata soko la ajira miezi sita kuanzia tarehe ambayo ombi lake la ulinzi lilipoingizwa, kama bado hajapokea pendekezo la kwanza kutoka katika Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa, na kama ametoa ushirikiano kwa mchakato.

Waombaji wanaokidhi vigezo wanaweza kutuma maombi kwa Waziri wa Sheria ili kupata ruhusa ya kuingia katika soko la ajira, ambayo inaruhusu kuajiriwa na kujajiri. Mwombaji ambaye bado hajapokea maamuzi ya pendekezo la kwanza la maombi yake ya ulinzi ndani ya kipindi cha miezi 5 anaweza kutuma maombi ya kuweza kuingia katika soko la ajira. Ruhusa hiyo, kama ikitolewa, itaanza kutumika kama mwombaji bado ana vigezo tarehe ambayo ipo miezi 6 kuanzia siku waliyotuma maombi yao ya ulinzi wa kimataifa.

Kitengo cha Upataji wa Masoko (LMAU) ambacho ni sehemu ya Huduma ya Uhamiaji (ISD), wanashughulikia maombi kwa niaba ya Waziri wa Sheria. Ruhusa ya miezi 12 inatolewa kwa waombaji waliokidhi vigezo na inatolewa tena upya mpaka pale kutakapokuwa na uamuzi wa mwisho juu ya ombi la mwombaji.

Waombaji wenye vigezo wanauwezo wa kuingia katika sekta zote za ajira, kasoro katika Utumishi na Huduma za Umma, Garda Siochana, na katika Vikosi vya Ulinzi vya Ireland.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu ya Uraia Asili wa Ireland na Huduma za Uhamiaji:
<http://www.inis.gov.ie/en/INIS/Pages/labour-market-access>

Tafadhali kumbuka kwamba baadhi ya taarifa zinazotolewa kwa madhumuni ya maombi ya ulinzi wa kimataifa zinaweza kutolewa kwa Watoaji wa Huduma za Uhamiaji na baadhi ya Vitengo vya Serikali, kulingana na sheria, kwa malengo ya utekelezaji wa maombi kwa ajili ya kutoa idhini ya kuingia katika Soko la Kazi.